**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA MAONESHO YA TANO YA BIDHAA ZA VIWANDA VYA TANZANIA KATIKA UWANJA WA MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA WA MWALIMU J. K. NYERERE, DAR-ES-SALAAM TAREHE 4 DESEMBA, 2020**

- Mheshimiwa Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,
- Ndugu Prof. Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu , Wizara ya Viwanda na Biashara,
- Ndugu Ludovick Nduhiye, Naibu KM, Wizara ya Viwanda na Biashara,
- Ndugu Dkt Jim Yonaz, NaibuKatibu Mkuu Mawasiliano,
- Ndugu Edwin N. Rutageruka, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE),
- Ndugu Paul Mshimo, KatibuTawala Mkoa wa Dar es Salaam
- Bibi Latifa M. Khamisi, Naibu Mkurugenzi Mkuu - Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania,
- Mheshimiwa Godwin Gondwe, Mkuu wa Wilaya ya Temeke,
- Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali mliopo hapa,
- Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa,
- Menejimenti na Wafanyakazi wa TanTrade,
- Washiriki wa Maonesho,
- Wasanii, Kwaya ya Chuo cha Utumishi wa Umma,
- Waandishi wa Habari,
- Wageni Waalikwa,
- Mabibi na Mabwana. **Habari za asubuhi!**

## SHUKRANI

**Awali ya yote**, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sote kukutana hapa leo hii tukiwa na afya njema. Aidha, naishukuru Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Maonesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania.

**Pili,** naomba nitumie fursa hii kuwaletea salaam za dhati za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na salamu kutoka kwa Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais. Viongozi wetu hao, wametoa pongezi nyingi sana kwa kufanikisha maonesho haya ya bidhaa za viwanda kwa mwaka 2020. Mtakubaliana nami kwamba bidhaa nyingi zilizopo katika maonesho haya zimetokana na maono na uongozi mahiri na shupavu wa Rais wetu mpendwa katika kipindi chake cha kwanza cha kuongoza Serikali ya awamu ya tano.

**Tatu**, Kwa niaba ya Serikali, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania wote kwa ujumla wao kwa imani yao kubwa kwa Chama chetu cha Mapinduzi na kwa kukipa tena ridhaa ya kuwatumikia watanzania. Ushindi wa kishindo wa kura nyingi alizopata Mheshimiwa Rais na Wabunge wote wa CCM ni ishara tosha kwamba watanzania wana imani kubwa na Serikali yao kutokana na kushuhudia maendeleo makubwa na ya haraka kupitia sera makini na utelekezaji wa vitendo wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015 - 2020.

Nawashukuruni sana na ninaahidi kama Mtendaji Mkuu wa Serikali nitaendelea kushirikiana na wananchi wote wa Tanzania katika kutekeleza yale yote tuliyoyaahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025 kwa maendeleo ya Taifa letu.

**Nne:** kipekee, nachukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara na Uongozi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kwa kufanikiwa kuandaa Maonesho ya Bidhaa za Viwanda kwa **miaka mitano mfululizo**. Hii ni hatua nzuri itakayowezesha bidhaa za viwanda vyetu kupata soko endelevu la ndani na nje ya Nchi. Aidha, niipongeze Kamati ya Kitaifa ya maandalizi ya maonesho haya kwa kazi nzuri inayoonekana ya kuandaa kwa mafanikio makubwa.

Kwa namna ya pekee natoa pongezi nyingi sana kwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania kwa kuendelea kuratibu vema maonesho haya, ambayo yameendelea kukua na kupata washiriki wengi ukilinganisha na yalipoanza mwaka 2016. **Hongereni sana!**

**Tano:** nitumie fursa hii pia, kuwashukuru Wageni Waalikwa mbalimbali wakiwemo Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Wananchi pamoja na Wawakilishi wa Vyombo vya Habari ambao kwa ujumla wao wamefika kutuunga mkono katika hafla hii ya ufunguzi wa maonesho haya.

## KAULIMBIU YA MAONESHO YA TANO YA BIDHAA ZA VIWANDA

**Ndugu wananchi,** maonesho haya yalianzishwa mwaka 2016 kufuatia maelekezo yaliyotolewa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, yafanyike Maonesho ya Bidhaa za Viwanda ili kuwezesha bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu zipate masoko ndani na nje ya nchi. Nafarijika kuona kuwa agizo la Mheshimiwa Rais limetekelezwa kwa viwango vya kuridhisha.
**Hongereni sana na endeleeni kuyaboresha!**

Nilipowasili kwenye eneo hili, nilipata fursa ya kutembelea baadhi ya mabanda ya maonesho. Wakati natembelea mabanda hayo, nimefarijika kuona bidhaa nzuri na zenye ubora zilizotengenezwa na viwanda vyetu. Nawapongeza sana wazalishaji kwa kuendelea kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango. Aidha, nazipongeza Taasisi zetu zinazotoa huduma wezeshi kwa viwanda vyetu kwa kuendelea kutoa msukumo na ushauri wenye tija wa kukuza sekta ya viwanda.

Katika mabanda mengi, nikiri kwamba nimevutiwa na kuwepo kwa bidhaa mpya na bora. Aidha, pamoja na mambo mengine nimeona mwitikio mkubwa wa wadau kutoka mikoa mbalimbali Nchini. Hivyo, natoa pongezi na shukrani kwa wadau wote wapya mliojumuika nasi katika maonesho haya ya mwaka huu wa 2020 ikiwemo wale wanaotoka mikoani.

**Ndugu Wananchi,** eneo lingine lililonivutia kwenye maadhimisho haya ya mwaka huu ni Kaulimbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu wa 2020 inayosema **"Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania**". Kaulimbiu hii imebeba maono na sera ya Serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa viwanda. Vilevile, Kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha uzalendo mshikamano na utaifa na inatukumbusha kuwa maendeleo ya kiuchumi yanahitaji mapinduzi ya kifikra. Kwa msingi huo naamini Wadau wataitumia Kauli mbiu hii kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwemo za Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Misitu na Madini kwani kutokana na Mkakati wetu wa kitaifa, viwanda vingi vinatumia mali ghafi za ndani.

**Ndugu wananchi**, nipende kusisitiza kwamba kutumia bidhaa tunazozalisha kutoka viwanda vyetu kutaisaidia Tanzania kufikia hatua ya juu ya Uchumi wa Kati. **Hivyo basi**, nitoe rai kwa Watanzania kutekeleza kwa Vitendo Kauli Mbiu ya Maonesho haya inayosema **"Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania**". Utekelezaji wa kaulimbiu hii utakuwa ni muarobaini wa kuchochea ukuaji wa viwanda na biashara hapa Nchini.

Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali inathamini sana mchango mkubwa wa viwanda katika kuinua uchumi. Kwa kutambua hilo, nitoe wito kwa wenye viwanda wote hapa nchini kushiriki ili kuwawezesha Wananchi kuona bidha bora na mpya zinazozalishwa Tanzania.

## UMUHIMU WA MAONESHO YA BIDHAA ZA VIWANDA

**Ndugu Washiriki**, maonesho haya ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania ni fursa muhimu kwa Wadau wote wakiwemo wazalishaji wa bidhaa viwandani, wafanyabiashara, taasisi mbalimbali za umma, makampuni na watu binafsi kukutana na kubadilishana mawazo na uzoefu chini ya mwamvuli mmoja.

Nimefarijika sana kuona mmefika kwa wingi katika maonesho haya, hali hii inaashiria na kuonesha kuwa mmeamua kwa dhati kutoa fursa kwa wananchi kuweza kujionea uwezo mkubwa wa Watanzania wa kuzalisha mashine na bidhaa bora kama nilivyojionea wakati natembelea kwenye maonesho haya. Maonesho ya viwanda vya ndani yana umuhimu wa pekee kwani Kupitia maonesho haya tunapata manufaa mengi yakiwemo yafuatayo;

- wawekezaji kupanua wigo wa masoko ya bidhaa na kuwezesha kupanuka kwa viwanda kutokana na kupanuka kwa masoko;
- kubadilishana mawazo, ujuzi na uzoefu chini ya mwamvuli mmoja na hatimaye baada ya maonesho kuboresha bidhaa kulingana na mahitaji ya walaji au soko;
- kupata taarifa ya masoko ya bidhaa zinazozalishwa na kujifunza mambo mbalimbali kutoka miongoni mwenu na kutoka kwa Taasisi zilizoshiriki kwenye maonesho;
- nyenzo muhimu ya kukuza biashara na uchumi kwa kuwatambulisha na kuwakutanisha Wazalishaji, Wanunuzi na watumiaji kwa pamoja;

- Fursa ya Kuingia na kufunga mikataba ya kibiashara pamoja na kupata miadi (order) ya bidhaa na kuwashawishi na kuvutia wawekezaji kuendelea kuwekeza kwenye viwanda;

- kutoa mrejesho wa ubora wa bidhaa mnazozalisha ili kuwawezesha kubaini changamoto zinazowakabili kwa pamoja na kuona namna ya kuzitafutia ufumbuzi;

- kuwafungua macho wananchi kuona na kutambua teknolojia, bidhaa na huduma zinazopatikana hapa nchini kutokana na maendeleo ya sekta ya viwanda vya ndani na;

- kupanua wigo wa ushirikiano miongoni mwa wawekezaji na pia kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika kuendeleza viwanda;

- kupata undani wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kudadisi kuhusu huduma zinazotolewa na taasisi mbali mbali zilizopo hapa uwanjani;

- Hii pia ni sehemu ya jukwaa la kutangaza fursa za kiuchumi na kijamii za nchi yetu kwa lengo la kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kupitia fursa ya Mikutano ya ***online B2B*** itakayofanyika hivi karibuni. Naamini mikutano hiyo itakuwa na tija kwa washiriki, kwa hiyo ni vyema tukaitumia fursa hii kikamilifu. Naamini TanTrade mmejipanga vizuri na mtatupatia mrejesho.

Hivyo, nitumie fursa hii kwa mara nyingine kuwashukuru wazalishaji na wafanyabiashara walioonesha bidhaa zao hapa; Wadhamini, Wananchi na wageni wote waliofika na kutembelea maonesho haya kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu. Ushiriki wenu unadhihirisha imani yenu katika kuunga mkono juhudi za Serikali ambazo zimeainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025 ya kujenga uchumi jumuishi kwa lengo la kuinua kipato cha Mtanzania.

**Ndugu wananchi,** ninatoa wito kwa Watanzania wenzangu kuja kutembelea Maonesho haya ili kutambua na kuzipenda bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu pamoja na fursa za Sekta hii ya Viwanda hapa nchini. Nami naunga mkono kaulimbiu ya maonesho **"Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania**".

## MIKAKATI YA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA WAWEKEZAJI KWENYE SEKTA YA VIWANDA NCHINI

Pamoja na jithada za Serikali kuweka mkazo mkubwa katika ujenzi wa Viwanda. Natambua kwamba Sekta Binafsi ndiyo muhimili mkubwa wa kujenga uchumi wa viwanda. Hivyo, Serikali itaendelea kuhamasisha na kushawishi wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kuhakikisha chngamoto mbalimbali zinafanyiwa kazi ipasavyo.

### Kuondoa Urasimu

**Mheshimiwa Wananchi,** serikali inaendelea kujenga mazingira rafiki kwa wawekezaji na kuondoa vikwazo visivyo vya lazima kama vile urasimu uliopitiliza. Natumaini mnakumbuka, Mheshimiwa Rais alipokuwa akilihutubia Bunge mnamo tarehe 13 Novemba 2020, pamoja na mambo mengine alitoa msimamo wa serikali kwamba kuanzia sasa anataka Wawekezaji wanapokuja nchini wapatiwe vibali vya kuwekeza ndani ya siku 14.

**Kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji na kufanya biashara;**
**Ndugu wananchi,** Serikali, inaendelea kurahisisha na kuweka mazingira mazuri ya ukuaji wa sekta hii. Kwa niaba ya Serikali yetu inayoongozwa na Mhe. Rais wetu Mpendwa Dkt.John Joseph Pombe Magufuli nawahakikishia kuwa changamoto zote ambazo zimegundulika kupitia wadau wa Maonesho haya tutazifanyia kazi ipasavyo.

**Kuendelea kufanya makongamano mbalimbali:**
Serikalli itaendelea kuratibu fursa mbalimbali za kuwakutanisha wazalishaji, wawekezaji na watumiaji wa bidhaa ili kuweza kujadili na kutatua changamoto mbalimbali.

Nimejulishwa kwamba **kesho, tarehe 5 Novemba, 2020** katika viwanja hivi kutafanyika mkutano maalum unaolenga kuwakutanisha Wakuu wa Taasisi za Umma za Udhibiti na Wenye Viwanda ili kupokea na kutatua changamoto zinazowakabili. Pia nimetaarifiwa kuwa, tarehe 7 Novemba kutakuwa na kongamano lingine la fursa za biashara na viwanda baina ya Tanzania na nchi za Pakistan, Kuwait, Dubai na Urusi.

Ni matarajio yangu kuwa kupitia mikutano hiyo wazalishaji wetu wataweza kujifunza kutoka kwa Washiriki wanaotoka nje ili kupata teknolojia mbalimbali za mashine za viwanda zikiwemo za uzalishaji, ufungashaji na usambazaji wa bidhaa.

Naagiza, Wakuu wa Taasisi za udhibiti wote walioalikwa washiriki mkutano huo watumie fursa hiyo kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji na wafanyabiashara wa sekta ya viwanda.

**Kufufua viwanda vilivyokufa kwa kuzingatia teknolojia ya kisasa:**
**Ndugu wananchi,** kutokana na mkakati wa ujenzi wa uchumi wa viwanda, kumekuwa na ongezeko la viwanda vipya kila mwaka licha ya kuwa vipo viwanda vichache ambavyo vinapungua kutokana na sababu mbalimbali kama vile kubadilika kwa teknolojia na mazingira ya ushindani. Serikali kwa kutambua hilo, imejiwekea mikakati ya kufufua viwanda vilivyokufa na kuongeza uzalishaji wa viwanda vilivyopo. Nipende kuwajulisha kuwa, Serikali imekuwa ikifuatilia sababu za kuanguka kwa baadhi ya viwanda nchini hatimaye kuchukua hatua ya kuviokoa kwa kutatua changamoto hizo zinazoikabili sekta hii ya viwanda.

**Kufanya mabadiliko na kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma** kwa kuunganisha taasisi zinazotoa huduma zinazofafa

**Kufanya mageuzi katika Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki**:
Aidha, tumeboresha mifumo mingi ya utoaji huduma katika taasisi mbalimbali za umma kuwa ya njia ya Kielektroniki. Huduma hizo ni pamoja na **Usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni** pamoja na **Utoaji wa Leseni** za **Biashara** zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, BRELA.

**Kupunguza mnyororo wa gharama za uzalishaji ili** kupunguza gharama za uzalishaji na kufanya bei ya bidhaa zinazozalishwa nchini na viwanda vyetu ziwe shindani.

**Wito kwa wawekezaji kutoka nje:**
Kutokana na mazingira haya ya uwekezaji na kwa kuzingatia hali ya Amani iliyopo ndani ya nchi yetu, napenda kuwakaribisha wawekezaji mbalimbali kutoka nje kuwekeza katika teknolojia ya viwanda hapa Tanzania, **tunawakaribisha sana** kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye rasilimali na malighafi

za kutosha kwa uzalishaji viwandani. Serikali ya Tanzania imeweka mikakati mahususi ya kuimarisha na kuendeleza sekta ya viwanda ili kuongeza ajira kwa wananchi na hivyo kuwapunguzia umaskini.

## MAENDELEO KATIKA KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA

**Ndugu wananchi,** uchumi wa nchi yetu umekuwa ukiimarika na kukua kwa wastani wa **asilimia 7** kwa mwaka. Hii ni kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kujenga miundombinu ya kiuchumi kama vile barabara, uimarishaji wa bandari, uimarishaji wa reli, na ukuzaji wa Sekta ya Mawasiliano, ukuzaji na uongezaji wa uwezo wetu wa kuzalisha na usambazaji wa nishati ya umeme.

**Ndugu Wananchi,** kama mnavyofahamu, Tanzania imeingia katika kundi la kipato cha kati kabla ya mwaka 2025 kama iliyowekwa bayana katika Dira ya Maendeleo ya **2025.** Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa ujenzi wa uchumi wa kipato cha kati ambao Tanzania imefanikiwa kuufikia mwaka huu, utaakisi sura na maisha ya Watanzania walio wengi. Moja ya njia mahsusi ya kutufikisha huko ni uendelezaji wa viwanda na uwajibikaji wa dhati kwa watendaji.

### Mkakati wa Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda:

Napenda kuwajulisha kuwa Serikali imetoa msukumo mkubwa na kuwezesha viwanda vingi kujegwa katika kipindi kifupi na hivyo kuwezesha idadi ya viwanda kuongezeka hadi kufikia viwanda **61,110** mwaka 2020 ikilinganishwa na viwanda **52,633** mwaka 2015. Hii ina maana kuwa viwanda **8,477 pekee** vimejengwa kati ya mwaka 2015 hadi 2019. Kati ya hivyo, viwanda vikubwa ni 201; viwanda vya kati ni 460 na viwanda vidogo na vile vidogo sana ni 4,410.

Aidha, viwanda hivyo vipya vimesaidia kuongezeka kwa ajira kutoka 254,786 (mwaka 2015) hadi kufikia ajira 482,601 (mwaka 2020).

Takwimu zinaonesha kuwa viwanda vingi vilivyosajiliwa kwa kipindi hiki ni kwa ajili ya kuzalisha vigae, marumaru, saruji, sabuni, sukari, sigara, nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi, chuma na bidhaa za chuma, kusindika nyama, chakula, mbogamboga na matunda, maziwa, mafuta ya kula, vifungashio, mbolea, dawa za binadamu na vifaa kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwemo corona (COVID 19) pamoja na viwanda vya ubanguaji wa Korosho.

**Ndugu Wananchi,** Serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda ambavyo sehemu kubwa ya malighafi zake zinatoka ndani ya nchi yetu, hususan kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini – na maliasili nyingine. Viwanda vya aina hii vitatupa fursa ya kujenga mfumo wa uzalishaji wa ndani ya Nchi uliofungamana na kuendana na mahitaji ya soko. Wazalishaji watakuwa na soko la uhakika humu humu ndani ya nchi. Viwanda vingine ambavyo tutawekeza ni vya kuzalisha bidhaa ambazo zinatumiwa na watu wengi humu nchini *(mass consumption)* – yaani bidhaa kama vile nguo, viatu, mafuta ya kupikia, zana za kilimo, vifaa vya ujenzi, pembejeo kwa wakulima, n.k.

Hivyo basi, viwanda hivi vitakuwa na uhakika wa soko la ndani kabla ya kufikiria soko la nje na vinatarajiwa kuzalisha ziada kwa ajili ya masoko ya nje. Mambo yote haya yakifanyika, yaani kuzalisha kwa ajili ya soko la ndani na nje, itatuongezea akiba yetu ya fedha za kigeni na kutuwezesha kutekeleza na kuendeleza mipango mingine kwa ajili ya ustawi wa uchumi wetu.

Serikali yetu imeweka vivutio maalumu kwa wawekezaji wa ndani kama njia ya kuwahamasisha Watanzania kuwekeza katika nchi yao. Serikali itaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara katika azma ya kukuza sekta ya Viwanda na biashara Nchini. Lengo ni kuwezesha Tanzania kufikia hatua ya juu ya uchumi wa kati kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025.

**MAAGIZO NA MASUALA YA MSISITIZO:**

**Ndugu Washiriki**, ninayo imani kubwa kuwa kwa njia ya maonesho ya bidhaa za viwanda vya ndani tutaweza kuondoa imani potofu kuwa kitu bora ni kile kilichotoka nje ya nchi. Imani hii ikiondoka itasaidia sana uzalishaji mkubwa wa bidhaa na teknolojia hapa nchini ambazo zitawezesha kupata masoko ya ndani na nje.
Nina hakika tukijipanga tutaweza kuwa washindani mahiri na bidhaa zenu zitaingia na kuleta ushindani mkubwa kwenye soko. Hata hivyo masuala yafuatayo ya msisitizo na maagizo ni muhimu sana yakafanyiwa kazi kikamilifu;

i. Wenye Viwanda zalisheni bidhaa kwa wingi na kwa kutumia malighafi zinazopatikana kwenye maeneo yenu, hii itawezesha kuwa na uzalishaji wenye gharama ndogo na kuwa na bei shindani katika soko. Kumbukeni kuwa, bidhaa ikizalishwa kwa kutumia mali ghafi zetu itawezesha ajira endelevu kuwepo kwa vijana wetu, itasaidia pia malighafi zetu kutoharibika lakini pia bidhaa zetu zitakuwa zina thamani kubwa badala ya kuuza malighafi kwa bei ya chini.

ii. Uwekezaji unaofanywa uzingatie uendelevu, ubora na tija kulingana na viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa katika shughuli za uzalishaji ili kuhimili ushindani na hata kuweza kunufaika na fursa za masoko zinazoendelea kujitokeza,

iii. Mamlaka zote za udhibiti hakikisheni kuwa bidhaa zisizo na viwango na bidhaa bandia hazipati nafasi ya kuingia soko la Tanzania. Hii iende sambamba kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kuoneshwa katika Maonesho mbalimbali zinakuwa na viwango vya kimataifa ili kuvipa changamoto viwanda vya ndani kuzalisha bidhaa zenye ubora.

iv. Wazalishaji na wenye viwanda hakikisheni mnazitangaza bidhaa zenu (marketing) na kuzalisha bidhaa zenye kuzingatia ubora na mnyororo wa gharama ili ziweze kushindana katika soko;

v. Wawekezaji na wazalishaji wote wote tufanye biashara halali, tulipe kodi kikamilifu na kutunza kumbukumbu vizuri ili Serikali iweze kupata takwimu sahihi za biashara zinazofanyika ikiwemo na nchi jirani ili kuweza kuandaa sera mahususi za kuwasaidia.

vi. Wizara ya Viwanda na Biashara hakikisheni wazalishaji wanatumia vizuri sheria za uasilia wa bidhaa ili kuweza kukidhi matakwa na kutumia fursa ya masoko ambayo Serikali yetu imesaini mikataba ya maridhiano hususani soko la Afrika Mashariki, SADC, AGOA na fursa nyingine za masoko ya pamoja.

vii. Watanzania tuachane na fikra potofu kuwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi ndizo zenye ubora kuliko za hapa nchini, kwani bidhaa zetu ni bora na zina viwango vinavyostahili. Hebu sote tununue bidhaa zetu ili kukuza ajira na pato la mtu binafsi na Taifa kwa ujumla.

viii. Wizara ya fedha na Mipango na Viwanda na Biashara endeleeni na mikakati ya kisera na kikodi ya namna ya kupunguza uagizaji wa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nje na kuongeza ununuzi wa bidhaa zinazozalishwa ndani ili kukuza viwanda vya ndani mfano; bidhaa za mbao, mafuta ya kula, nk.

ix. SIDO kwa kushirikiana na VETA wekeni kipaumbele cha kutoa mafunzo na kubuni nyenzo zinazoendana na mahitaji makubwa yaliyomo katika jamii ikiwemo katika eneo la kuchakata mazao kama korosho, chikichi, ufuta, alizeti na matumizi ya TEHAMA katika kuboresha uzalishaji mali, ufanisi, viwango na kutafuta masoko,

x. Wizara ya Viwanda na Biashara na TANTRADE fanyeni maboresho katika uratibu wa maonesho mbalimbali ya Viwanda na Biashara ili yafanyike kwa kuzingatia kanda za uzalishaji nchini badala ya nguvu kubwa kuelekezwa Dar Es Salaam na miji mikubwa. Ili Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda ushamiri vya kutosha, lazima kuwe na na mfungamano na sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini ili kutoa malighafi za kutosheleza viwanda hivyo. Lazima kuwe na msukumo wa kutosha kwenye sekta zinazozalisha malighafi.

xi. TANTRADE iendelee kushirikiana na Balozi zetu ili kuendelea kupata fursa za masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini.

xii. Halmashauri zote Nchini zihakikishe Viwanda vilivyo katika Mamlaka zao vinashiriki kuonesha bidhaa wanazozalisha ili bidhaa hizo ziweze kutafutiwa masoko katika Nchi mbalimbali duniani zikwemo nchi za Ukanda wa EAC na SADC kwa lengo la kuongeza mauzo ya Tanzania nje ya nchi.

xiii. Ufuatiliaji ufanyike kujiridhisha kuwa Halmashauri zote nchini zimetekeleza maagizo ya kuweka kipaumbele katika kutenga, kurasimisha, kupima na kuyawekea miundombinu maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, madini, uvuvi na viwanda vidogo,

**MWISHO**

Nawapongeza sana TanTrade kwa kuandaa Siku Maalum sambamba na Maonesho haya mahususi kwa ajili ya Kongamano la Wafanyabiashara wenye Viwanda na Taasisi za Uthibiti ambalo litafanyika kesho Jumamosi. Kongamano hili ambalo nimeambiwa limeandaliwa na TANTRADE kwa Udhamini wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ni mojawapo ya juhudi za Serikali za kuendeleza ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) katika kujadili kwa pamoja changamoto za Sekta ya Viwanda ili kuzipatia ufumbuzi na hatimaye sekta hii iendelee kushika kasi ya ukuaji.

Aidha, Serikali kwa upande wake itaendelea kuhakikisha kuwa inatoa msukumo na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na TANTRADE ili kuinua kiwango cha uzalishaji wa mali ghafi na kutafuta masoko ya bidhaa za Viwanda vyetu.

Ni imani yangu kuwa utaratibu huu utakuwa endelevu kwani utasaidia kwa kiasi kikubwa kuyafanya maonesho haya kuendelea kuwa na mtazamo mpana na Mzuri na pia kuchangia katika kukuza biashara na uwekezaji baina yetu. Natoa wito kwa WenyeViwanda na Wadau wote muhimu kushiriki na kuitumia fursa hii vema. Msisitizo huu wafanyabiashara pia tuimarishe biashara zetu.

**Ndugu Wananchi,** Nitafarijika sana kuona Maonesho haya yakiendelea kutumika kama jukwaa la kufanya kampeni za makusudi kuhamasisha Watanzania kuthamini na kuzipenda bidhaa zinazozalishwa nchini. Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba "**Maonesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania kwa mwaka 2020"** yamefunguliwa rasmi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**